

TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI YA UWAKALA WA USAFI WA MAZINGIRA HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

1. Halmashauri ya Mji wa Bunda inakusudia kupata wazabuni wenye uwezo wa kufanya Usafi wa Mazingira, Kuzoa taka na kuzisafirisha kwenda dampo la Migungani kutoka katika maeneo ya Makazi, Biashara, Masoko, Maeneo ya wazi na Taasisi mbalimbali katika Halmashauri ya Mji wa Bunda kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Agosti 2023 hadi tarehe 1 Agosti, 2024
2. Halmashauri ya Mji wa Bunda inapenda kuwaalika **wakandarasi, Watu Binafsi, Makampuni, Mashirika, Vikundi au Taasisi za umma zilizosajiliwa kisheria**, wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo kutuma maombi yao kwa zabuni kama ifuatavyo :-

A: UWAKALA WA USAFISHAJI WA MAZINGIRA utajumuisha kata zifuatazo;

- Bunda Mjin (Mitaa ya Mapinduzi, Posta na Nyerere),
- Kabarimu (Mitaa ya Majengo, Kilimahewa, Nyiendo, Saranga na Kabarimu)
- Nyasura (Mitaa ya Zanzibar, Makumbusho, Nyasura A, Nyasura B, Nyasura C, na Nyasura D)
- Kata ya Nyamakokoto (Mitaa ya Kabusule, Mburumatale, Majengo mapya, na Ukerewe road)
- Balili (mitaa ya Rubana na Balili)
- Manyamanyama (Mitaa ya Katoliki, Shuleni, Mbungani)
- Bunda stoo (Mitaa ya Miembeni, Kilimani, Idara ya maji, Migungani na Butakale)

KUMBUKA

Mwombaji anatakiwa kuomba zabuni ikijumuisha kata zote zilizo tajwa hapo juu.

MASHARTI YA JUMLA KWA ZABUNI ZOTE

1. Nakala ya leseni hai (isipokuwa CBO's hazihusiki na sharti hili).
2. Waombaji wote waambatanishe nakala za usajili wa Makampuni yao au Vikundi vya Kijamii (CBOs) au Taasisi.
3. Vikundi vya Kijamii (CBOs) viambatanishe orodha ya viongozi wa kikundi na barua za utambulisho kutoka katika Kata husika.
4. Waombaji wote waambatanishe nakala za VAT au TIN.

3. Vikundi vya Kijamii (CBOs) viambatanishe orodha ya viongozi wa kikundi na barua za utambulisho kutoka katika Kata husika.
4. Waombaji wote waambatanishe nakala za VAT au TIN.
5. Mwombaji ni lazima aambatanishe wasifu wa kampuni (Company Profile) au Kikundi CBO's Profile au taasisi.
6. Waombaji wawe na vithibitisho vya kuwa na vifaa vya kazi kama magari/Trekta kwa kusafirishia taka kwenda dambo, Vifaa vya kutosha vya kusafishia, wafanyakazi/vibarua wa kutosha kutokana na ukubwa wa eneo, pamoja na ofisi ya kudumu. Au aeleze kwa kuambatanisha uthibitizo kuwa amekubaliwa kukodi, magari ya Halmashauri ya Mji wa Bunda
7. Ili kuhakikisha afya na usalama kwa wafanyakazi watatakiwa kupima afya zao mara mbili kwa mwaka na pia wawe na vifaa kinga "personal protective equipments" (kama vile;-Vizuia harufu mbaya).
8. Muombaji/waombaji anatakiwa kuwasilisha picha za Mkurugenzi /Wakurugenzi/Meneja /Mwenyekiti/Katibu wa kampuni yao katika maombi yao.
9. Kamati ya tathimini itakagua ofisi, magari ya kusafirisha taka, vifaa vya usafi, vielelezo mbali mbali vilivyo tajwa hapo juu vya mwombaji, na kutoa mapendekezo kwa kitengo cha manunuzi.
10. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Mji wa Bunda. Aidha, mwombaji aliyewahi kushitakiana na Halmashauri ya Mji wa Bunda kuhusiana na kazi yeyote, hatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi yeyote ya zabuni iliyotangazwa na Halmashauri ya Mji wa Bunda. Vile vile Waombaji watakaothibitika kuwa na tuhuma za utendaji usiozingatia Sheria kutoka Taasisi nyingine za Serikali hawatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi zinazotangazwa na Halmashauri ya Mji wa Bunda.
11. Mwombaji yeyote atakayeshindwa kutimiza au kutokamilisha maelekezo na masharti hayo ya zabuni atakuwa amejiondoa mwenyewe katika ushindani.

12. Halmashauri ya Mji wa Bunda hailazimiki kukubali/ kutokubali kutoa [Award Tender] zabuni kwa mwombaji kutokana na kigezo cha malipo makubwa ya kazi ama huduma iliyoombewa zabuni.
13. Mzabuni atakayeshinda zabuni atatakiwa kuweka dhamana (bond) ya makisio ya makusanyo ya miezi mitatu (3). Dhamana hiyo itarudishwa baada ya mkataba kuisha, na endapo mzabuni atashindwa kutimiza masharti ya mkataba dhamana hiyo itatumika kutekeleza shughuli za sehemu ya mkataba mpaka atakapopatikana mzabuni mpya.
14. Kabrasha la zabuni litatolewa kuanzia tarehe 10/5/2023 siku za kazi na saa za kazi hadi tarehe 31/5/2023
15. Zabuni zote zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri [seal], na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja zabuni, na namba ya zabuni na zipelekwe katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Mji wa Bunda. Juu ya bahasha iandikwe zabuni anayo omba. Maombi yote yatumwe kwa: **KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA. S.L.P 219, BUNDA.**
16. Tarehe ya mwisho wa kupokea maombi ni siku ya **Jumane ya tarehe 31 mwezi Mei mwaka 2023 Saa 4.30 Asubuhi** na ndiyo siku ya ufunguzi wa zabuni hizi. Waombaji au wawakilishi wao watakaopenda kuhudhuria ufunguzi wanaruhusiwa kuhudhuria.
17. Maombi yatakayofika baada ya muda uliowekwa kuisha hayatapokelewa na hayatafunguliwa.

Emmanuel J. Mkongo

**MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
BUNDA**